

## Mikakati Inayopendekezwa na Euphrase Kezilahabi katika Kukabiliana na Dhana Potofu Zilizopandikizwa na Wageni kuhusu Afrika na Mwafrika

Alfred Malugu<sup>1</sup>, Ernest Sangai Mohochi<sup>2</sup> na Mugyabuso Mlinzi Mulokozi<sup>3</sup>

<sup>1</sup>Chuo Kikuu cha Rongo

<sup>2</sup>Chuo Kikuu cha Kibabii

<sup>3</sup>Chuo Kikuu cha Dar es Salaam

### Ikisiri

Suala la dhana potofu kuhusu Afrika na Mwafrika lina historia ndefu sana. Historia yake inaweza kutazamwa kuanzia kipindi cha ukoloni. Dhana hizo potofu kuhusu Afrika na Mwafrika zilijengewa msingi wake sio tu katika vitabu vya dini kama vile *Biblia Takatifu*, bali pia kwa wanafalsafa na wasomi maarufu wa kale wa Kimagharibi kama vile Carl Meinhof na Georg Hegel. Dhana potofu zilizopandikizwa zilichochea kutawaliwa kwa Waafrika na Afrika kwa jumla. Kwa mfano, kwa kupitia *Biblia Takatifu* kuna hoja kuwa masaibu, shida, majanga na mambo mbalimbali yanayomsibu Mwafrika yanatokana na kulaaniwa. Kutokana na kuwapo kwa dhana potofu, makala hii inakusudia kutathmini mikakati mbalimbali inayopendekezwa na Euphrase Kezilahabi katika kukabiliana na dhana hizo. Mikakati hiyo itabainishwa kupitia riwaya za Kezilahabi za *Gamba la Nyoka*, *Nagona* na *Mzingile*. Aidha, katika kubainisha dhana hizo, tutaongozwa na baadhi ya mihimili ya Nadharia ya Ubaadaukoloni. Hii ni Nadharia inayofungamanishwa na Edward Said hususani baada ya kuandika kitabu chake cha *Orientalism* (1978).

**Maneno Muhimu:** Historia, Dhana Potofu, Afrika, Mwafrika, Mikakati, Ubaadaukoloni

### Utangulizi

Afrika na Mwafrika ni dhana ambazo zina historia ndefu sana. Historia yake inaweza kutazamwa kuanzia kipindi cha ukoloni. Dhana hizo potofu kuhusu Afrika na Mwafrika zilijengewa msingi wake sio tu katika vitabu vya dini kama vile *Biblia Takatifu*, bali pia kwa wanafalsafa na wasomi maarufu wa kale wa Kimagharibi kama vile Meinhof na Hegel. Kwa mfano, kupitia *Biblia Takatifu* kuna hoja kuwa masaibu, shida, majanga na mambo mbalimbali yanayomsibu Mwafrika yanatokana na kulaaniwa. Kulaaniwa kwa Mwafrika katika *Biblia Takatifu* kunasemwa kufungamana na kisasili cha Kiebrania kinachomhusu Nuhu na wanawe. Kisasili hicho kinabainisha kuwa Nuhu alikuwa na wana watatu ambao ni Shemu, Hamu na Yafethi. Miongoni mwa watoto hao, mmoja ambaye ni Hamu, alilaaniwa na baba yake (*Biblia Takatifu*, 1997, *Mwanzo* 9-10, uk. 8). Mtoto wa Hamu aliyelitwa Kanaani ndiye anaelezwa kuwa alikuja kuishi Afrika na kuanzisha ukoo wake. Kwa kuwa baba yake Kanaani, yaani Hamu, alikuwa amelaaniwa, ni dhahiri kuwa uzao wote wa Kanaani, yaani Waafrika, walikuwa wamelaaniwa. Maelezo haya yalitumiwa kama nyenzo ya kuhlalisha Mwafrika kupuuzwa na hata kuonekana ni mtu aliyelaaniwa.

Vilevile, dhana potofu kuhusu Afrika na Mwafrika ziliendelea kujengwa na wasomi maarufu wa Kimagharibi. Kwa mfano, Meinhof (1915) katika *An Introduction to the Study of African Languages* anazichukulia lugha za Kiafrika kama lugha za kishenzi. Meinhof anadai kuwa, haoni sababu ya mtafiti wa kisayansi, afisa, mfanyabiashara au mmisionari kujifunza lugha za washenzi katika makoloni yao, labda tu wajifunze iwapo washenzi hao hawajui lugha ya Mzungu. Na watalazimika kujifunza kwa minajili ya kuwasiliana na washenzi hao. Naye Hegel (1956) katika *The Philosophy of History* kwa upande wake, anaeleza kuwa Waafrika ni watu ambao hawakuwa na historia yao wenyewe. Aliwachukulia Waafrika sawa na watoto waliodumaa akili ambao hawangeweza kujiongoza wenyewe bila kuongozwa.

Wakoloni nao, kwa upande wao, walitoa mchango mkubwa katika ujenzi wa dhana potofu kuhusu Afrika na Mwafrika. Wakoloni hao walifanya masuala mbalimbali yaliyoSababisha kujengeka kwa dhana hizo potofu. Miongoni mwa masuala hayo ni kuleta lugha zao za kigeni na kuzikandamiza lugha za Waafrika. Kulingana na Mnyampala (1971) anaeleza kuwa, wakoloni waliotutawala walikita mamlaka yao na kutuletea kila hila na hivyo mila zetu kudharaulika. Mnyampala (keshatajwa) anahimiza kuiondoa lugha ya Kiingereza kwani anaiona ni lugha inayoifuja lugha ya Kiswahili. Shutuma zake amezelekeza katika msisitizo uliowekwa katika matumizi ya lugha ya Kiingereza ambapo lugha ya Kiingereza ndio lugha iliyohalalishwa kuwa lugha ya ofisini na kwa hivyo mtu ambaye hakuifahamu alidharauliwa na kuonekana mpumbavu. Maelezo kama haya ya Mnyampala (keshatajwa) yamefanana na mawazo ya Omari (1981), Kezilahabi (1993), Senkoro (1993) lakini pia Iribemwangi na Mukhwana (2011).

Kutokana na kuwapo kwa dhana potofu zilizopandikizwa na wageni kuhusu Afrika na Mwafrika, makala hii inatathmini mikakati mbalimbali inayopendekezwa na Euphrase Kezilahabi katika kukabiliana na dhana hizo potofu. Kwa kuwa isingekuwa rahisi kutathmini mikakati inayopendekezwa katika tanzu zote za fasihi, makala hii inatathmini mikakati hiyo katika riwaya ya Kiswahili. Riwaya zilizoteuliwa ni *Gamba la Nyoka*, *Nagona* na *Mzingile* zilizotungwa na Euphrase Kezilahabi. Tumeteua riwaya hizi kwa kuwa ni riwaya zilizotungwa kwa kufuatana. Pia, ni riwaya ambazo zinadhahirisha mikakati hii moja kwa moja. Aidha, tumependelea kumtumia Euphrase Kezilahabi kwa sababu toka kazi zake za mwanzo alidhahirisha kabisa kuwa miongoni mwa watu wanaopingana na dhana potofu zilizopandikizwa kuhusu frika na Mwafrika.

Njia iliyotumika katika kufanikisha utafiti huu ilikuwa ni mbinu ya uchanganuzi matini. Kulingana na Berg (2001), kuna tofauti ya uchambuzi matini katika utafiti wa kitakwimu na ule wa kitaamuli. Berg anaeleza kuwa mbinu hii huhusisha kutoa mahitimisho kutokana na kubainisha sifa za kipekee za ujumbe kwa utaratibu pasipo mapendeleo.

Katika uchanganuzi huo, kilichofanyika ni kusoma riwaya husika kwa makini ili kupata data muhimu na kisha kuanza kuzichanganua. Data zilizoshughulikiwa katika riwaya husika ni zile zinazohusiana na mikakati inayopendekezwa katika kukabiliana na dhana potofu kuhusu Afrika na Mwafrika tu. Data hizo zilichukuliwa katika riwaya tatu za Kezilahabi ambazo ni *Gamba la Nyoka*, *Nagona*, na *Mzingile*.

Sambamba na mbinu hiyo, Nadharia ya Ubaadukoloni ilitumika ili kutupatia data za utafiti tulizokuwa tunazihitaji. Nadharia ya Ungitamaduni/ki-Baadukoloni inafungamanishwa na wataalamu wanne ambao ndio wanatazamwa kama waasisi wa mwanzo kabisa waliochochea kuibuka kwa nadharia hii. Wataalamu hao ni: Edward Said, Homi Bhabha, Gayatri Chakravorty Spivak na Frantz Fanon. Kitabu cha Said cha *Orientalism* (1978) ndicho hasa kinachofungamanishwa na mawazo yaliyochochea kuibuka kwa nadharia hii.

Hata hivyo, katika miaka ya 1950, aliibuka Frantz Fanon ambaye ndiye alichukuliwa kuwa nguzo kuu ya uasisi wa nadharia hii ambapo aliandika kitabu chake cha *Black Skin, White Masks*. Aidha, katika miaka ya mwanzo ya sitini, Frantz Fanon alichapisha kazi yake maarufu ya *The Wretched of the Earth*. Neno hili “The Wretched” linatoka katika tafsiri ya neno la Kifaransa la “Les Damnes” lenye maana sawa na “The Cursed” katika lugha ya Kiingereza. Katika lugha ya Kiswahili, neno hili humaanisha “Waliolaaniwa.” Kwa hivyo, katika lugha ya Kiswahili, “The Wretched of the Earth” humaanisha “Viumbe Waliolaniwa.”

Njogu na Chimerah (1999) wanadai kuwa, uhakiki wa Baada-Ukoloni ni juhudi ya kuelewa uhusiano uliopo baina ya mataifa yaliyotawaliwa na yaliyotawala. Uhakiki huu unachunguza uhusiano baina ya nchi tawala na nchi tawaliwa, na kufichua unafiki uliokita katika madai ya usomi wa kilimwengu. Wataalamu hawa wanaendelea kusema kuwa, Nadharia ya Baada-Ukoloni ni ya kisiasa, na lengo lake ni kurejesha sifa na heshima ya lugha na fasihi za mataifa ya pembezoni. Ni juhudi za mataifa haya kurudi katika uasili wa mambo uliochafuliwa na ukoloni mkongwe. Maelezo kama haya yanapatikana pia kwa Wamitila (2002).

Kwa kadri muda ulivyoenda, nadharia hii iliendelezwa na baadhi ya wataalamu mbalimbali mmojawapo akiwa ni Mulokozi (2017). Mulokozi anadai kuwa, Ubaada-Ukoloni ni mtazamo unaosawiri, kuchambua na kukosoa hali ya mambo katika nchi zilizokuwa makoloni ya Ulaya hadi miaka ya karibuni, hususani nchi za Afrika, Asia na Karibiani.

Mulokozi (2017) anatubainishia mihimili muhimu ya nadharia hii. Mihimili hiyo ni: Kutambua na kutetea utambulisho wa Mwafrika, kuthamini lugha za asili na kuhimiza matumizi yake katika fasihi badala ya lugha za kigeni, kudai usawa na ukombozi kamili wa Mwafrika katika nyanja zote, kutetea mapambano ya uhuru wa Afrika nzima, kutetea ujenzi wa umoja na umajumui wa bara zima la Afrika, kutetea harakati za Wafrika wa Diaspora na mshikamano wao na Waafrika wa barani, kupinga usaguzi wa kitaifa na kijamii, usawiri hasi na potofu, na upuuzwaji wa Mwafrika na maono yake unaofanywa katika fasihi na vyombo vya habari vya nje ya Afrika, kupinga athari hasi za utandawazi unaompokonya Mwafrika hadhi, utu na rasilimali zake na pia, kuchunguza changamoto za umataifa na kuingiliana kwa tamaduni.

Miongoni mwa mihimili/misingi hiyo muhimu ya Ubaadakolonia iliyobainishwa na Mulokozi, katika utafiti wetu tulitumia mihimili miwili tu. Mihimili hiyo ni: Kwanza, kutambua na kutetea utambulisho wa Mwafrika. Pili, kuchunguza changamoto za umataifa na kuingiliana kwa tamaduni.

### **Maelezo Mafupi kuhusiana na Riwaya Teule**

Utafiti uliozaa makala hii, ulitokana na riwaya tatu teule. Riwaya hizo ni *Gamba la Nyoka* (1978), *Nagona* (1990) na *Mzingile* (1991). Riwaya hizi zimefuatana kimiaka katika uchapishaji wake na vinaonekana kuwa na mwendelezo kuanzia cha kwanza hadi cha mwisho.

Riwaya ya *Gamba la Nyoka* ni riwaya inayozungumzia utekelezaji wa vijiji vya ujamaa nchini Tanzania baada ya kutangazwa kwa sera hiyo. Licha ya sera hiyo kukusudiwa kuwa na tija kwa wananchi, mwandishi anaonesha utekelezaji mbovu wa sera hii. Ubovu huu unatokana na mambo yafuatayo: Moja, wananchi kutopewa elimu ya umuhimu wa uanzishwaji wa vijiji hivyo vya ujamaa. Pili, utekelezaji wa mabavu katika uhamishaji wa watu kuelekea vijiji hivyo vya ujamaa pamoja na kuwapo kwa uonevu na upendeleo. Na tatu, kutokuwapo na maandalizi madhubuti ya miundombinu muhimu katika vijiji hivyo walivyokuwa wanahamishiwa. Mbali na kuonesha utekelezaji wa sera ya uanzishwaji wa vijiji vya ujamaa, riwaya hii imezungumzia kwa kukosoa mambo mengine mbalimbali. Mambo haya ni kama vile: dini zilizoletwa na wageni, mtazamo hasi kuhusu uwezo wa akili ya Mwafrika, utamaduni wake, majina ya asili, historia yake, maendeleo na lugha za Kiafrika.

Kwa upande wa *Nagona* na *Mzingile*, riwaya hizi hutazamwa kama riwaya pacha. Baadhi ya watu ambao hawajabahatika kuziona, pindi wanapozisikia zikitajwa kwa pamoja, hudhani kuwa ni riwaya moja iitwayo *Nagona na Mzingile*. Kwa ufupi, mawazo yanayoanzia katika riwaya ya *Nagona*, yanaendelezwa katika riwaya ya *Mzingile*. Wazo kuu linalojitokeza katika riwaya hizi pacha ni lile la dhana ya 'ukweli.' Je, ukweli ni nini? Je, kuna ukweli mkamilifu? Na je, ukweli huo upo wapi au kwa nani? Maswali yote haya ndiyo msingi wa kuziangazia dhamira nyingine zote zinazopatikana katika vitabu hivi. Mbali na hayo, kama ilivyo riwaya ya *Gamba la Nyoka*, riwaya hizi zinabainisha mikakati mbalimbali inayopendekezwa na Euphrase Kezilahabi katika kukabiliana na dhana potofu zilizopandikizwa kuhusu Afrika na Mwafrika.

### **Mikakati ya kukabiliana na Dhana Potofu Zilizopandikizwa na Wageni kuhusu Afrika na Mwafrika**

Miongoni mwa dhana potofu zilizopandikizwa kuhusu Afrika na Mwafrika zimeegemezwa katika vipengele vya lugha, historia, maendeleo na utamaduni, akili, rangi ya ngozi na maumbile, na pia dini. Kutokana na dhana hizo potofu tulizozitaja zilizopandikizwa na wageni kuhusu Afrika na Mwafrika ambazo zimekuwa na athari mbalimbali kwa jamii za Waafrika, mwandishi Euphrase Kezilahabi anapendekeza mikakati mbalimbali katika kukabiliana na dhana hizo. Huku tukiongozwa na mihimili miwili tuliyoiteua, tulibaini kuwa Euphrase Kezilahabi anapendekeza kama ifuatavyo katika kukabiliana na dhana hizo potofu:

## Lugha

Kwa upande wa lugha, mwandishi haoni sababu ya Waafrika kutumia lugha za wageni katika shughuli zao mbalimbali. Anaona lugha za kigeni zinapotumika kwa wenyeji baada ya kuzipuuza lugha za wenyeji, lugha hizi zinaweza zisilieleweke. Kwa kutumia lugha hizi kwa mfano katika kufundishia kunaweka ugumu kwa wanafunzi kuelewa kile kinachofundishwa. Ndio maana katika riwaya ya *Mzingile*, mwandishi huyu katolea mfano wa mwalimu aliyejiua mwenyewe pale ambapo wanafunzi wake wa mawazoni waliposhindwa kujibu maswali yake kwa lugha ambayo alikuwa anaielewa yeye mwenyewe (uk. 25). Kutokana na mfano huu, ni dhahiri kabisa kwamba, Kezilahabi anapingana na matumizi ya lugha za kigeni katika elimu anayopatiwa Mwafrika. Hii ndio sababu ya wanafunzi wa mawazoni kutoweza kujibu maswali. Kezilahabi anapendekeza lugha za asili zitumike ili wanafunzi waweze kuelewa kile wanachofundishwa pamoja na kujibu maswali.

Vilevile, katika riwaya ya *Gamba la Nyoka* (uk. 95) mwandishi anapendekeza habari muhimu zinazomhusu Mwafrika zichapishwe pia katika lugha yake anayoelewa na sio kuchapishwa katika lugha za kigeni. Kutumika kwa lugha za kigeni ikiwemo lugha ya Kiingereza ni kasumba iliyopandikizwa na wageni, kwamba habari nzito zinapaswa ziandikwe kwa lugha ya kigeni kama vile Kiingereza. Kezilahabi anaonyesha jinsi lugha za kigeni zinapotumika katika kuandika habari nyeti zinavyowabagua baadhi ya watu katika kupata taarifa. Kwa mfano, Tinda anashindwa kuelewa lugha ngumu ya Kiingereza iliyotumika katika gazeti alilokuwa amekuja nalo Mamboleo. Kutokana na mfano huu, Euphrase Kezilahabi anasisitiza lugha za Kiafrika zitumike katika kufikisha ujumbe wa habari zinazowahusu Waafrika.

Katika kukabiliana na dhana potofu iliyopandikizwa kuhusu lugha za kigeni kama lugha bora dhidi ya lugha za Kiafrika, Kezilahabi anahimiza matumizi ya lugha za Kiafrika. Mkakati huu tunaanza kuuona hata katika diwani yake ya mwanzo kabisa ya *Kichomi*; diwani ya kwanza kabisa kuandikwa na Euphrase Kezilahabi. Kezilahabi haoni sababu ya kutumia lugha ya kigeni kwa watu wasemao lugha ya Kiswahili. Kwa hivyo, aliamua kuyatafsiri mashairi yake ambayo hapo awali alikuwa ameyaandika kwa lugha ya Kiingereza. Tukimnukuu anasema:

Kitabu hiki kimegawanyika katika sehemu mbili. Sehemu ya kwanza ni ya ‘Mashairi ya mwanzo.’ Mashairi haya yaliandikwa kwanza katika lugha ya Kiingereza, lakini hapa nimeyatafsiri kwa ajili ya mtu atakayetaka kuona jinsi nilivyoanza kujitosa katika ushairi. Baadaye sikuona sababu ya kuendelea kutoa mawazo yangu kwa watu wasemao lugha ya Kiswahili, kwa kutumia lugha ya kigeni. Baada ya kuandika shairi liitwalo ‘Kisu Mkononi,’ shairi langu la kwanza kuandikwa kwa Kiswahili, niliona kwamba lugha ya Kiswahili iliweza kutoa mawazo yangu vizuri zaidi. Nilianza kuandika na kufikiri kwa Kiswahili (uk. xiv).

Vilevile, Senkoro (1995) ni miongoni mwa wataalamu wanaotuthibitishia ni kwa vipi Kezilahabi alionelea matumizi ya lugha za asili kikiwemo Kiswahili kuwa ni mojawapo ya mikakati ya kukabiliana na dhana potofu kuhusu lugha ipaswayo kutumiwa na Waafrika. Senkoro anatuthibitishia kwa kurejelea kauli iliyowahi kutolewa na Kezilahabi miaka kadhaa iliyopita. Senkoro akimnukuu Kezilahabi anasema:

Leo, 1978, hapana haja ya mwandishi wa Kiswahili kujitetea. Mwandishi wa Kiswahili hana haja tena ya kujibu swali kama: Kwa nini ulikata shairi kuandika riwaya zako katika Kiswahili. Swali hili nimeulizwa mara nyingi. Siku hizi silijibu. Hali ilivyo sasa Afrika Mashariki, mwandishi anayepaswa kuwekwa jukwaani kujibu maswali ya umma ni yule anayeandika katika lugha ya wale waliomtawala, hapa Tanzania ikiwa ni lugha ya Kiingereza (uk. 61).

Maelezo hayo yanatuthibitishia ni nini msimamo au mtazamo wa Euphrase Kezilahabi kuhusu lugha ipaswayo kutumika katika mambo yanayowahusu Waafrika. Mawazo na mkakati huu umekuwa ni endelevu nao umejitokeza katika kazi zake nyingi. Mkakati kama huu pia ndio usisitizwao na Shaaban Robert 1954 kama alivyonukuliwa na Senkoro (1995), kwamba Shaaban Robert aliamua kutumia lugha ya Kiswahili ikiwa ni sehemu ya mkakati wa kurahisisha upataji wa maarifa. Uamuzi wa Robert kutumia lugha ya Kiswahili katika kuandika kazi zake ulilenga kuirahisisha jamii kupata

maarifa kwa lugha waliyoizoea (matiti waliyozoea). Ni katika mazingira kama hayohayo Robert (1966) anaifananiha lugha ya Kiswahili na titi la mama. Anasema titi la mama huwa ni tamu hata kama ni la mbwa. Anaweka msisitizo kwa Waafrika kutumia lugha zao pasipo kujali watu wengine wanawatazama vipi.

### Historia, Maendeleo na Utamaduni

Euphrase Kezilahabi katika riwaya zake teule, anapendekeza mikakati kadhaa inayohusiana na mambo ya historia, maendeleo na utamaduni. Katika kukabiliana na dhana potofu kuhusu Afrika na Mwafrika, anasisitiza kuandaa wataalamu wa Kiafrika ambao watatumika kuleta maendeleo katika nchi za Kiafrika. Mwandishi anaonelea kuwa, kwa kuwa tayari tuna vyuo vikuu, basi kinachotakiwa ni kwa vyuo vikuu hivyo kuwaandaa wataalamu watakaokuwa mstari wa mbele katika kuiletea maendeleo Afrika. Mkakati huu unadhihirishwa kupitia majibizano ya Mamboleo na Mambosasa kama anavyotuoonesha mwandishi katika riwaya yake ya *Gamba la Nyoka*:

Wataalamu tunao? Tusiwe tunasema maneno kutuliza masikio yetu yaliyozoea kusikia mihadhara ya wataalamu kutoka nchi za kigeni.” Unasema nini wewe! Tunacho Chuo chetu Kikuu. Tunacho kitivo cha uhandisi. Kinachohitajika ni kufundisha vijana hawa utaalumu unaohusiana na utengenezaji wa vyombo hivi, vyombo vya kilimo. Kwa njia hii wahandisi wetu watakuwa na umuhimu mkubwa katika kuharakisha mapinduzi tunayoyataka kuleta Tanzania. Kwa hiyo wataalamu tukiwa nao tutatengeneza vyombo hivi hapahapa nchini, badala ya kuchimba chuma na kupeleka Ulaya. Tutaendelea kulisha masoko ya viwanda vya Ulaya mpaka lini? Mambosasa! Tunahitaji *heavy industry*: Madini tunayo, reli tunayo, na watu wapo~akili, tunazo (kur. 43-44).

Maelezo hayo yanatuonyesha mikakati inayopendekezwa na Euphrase Kezilahabi katika kukabiliana na dhana potofu zilizopandikizwa kuhusu Afrika na Mwafrika. Mwandishi anaamini kabisa maendeleo ya nchi za Kiafrika yatatatikana pale Waafrika wenyewe watakapoachana na imani potofu kwamba Afrika haiwezi kupiga hatua ya kiviwanda pasipo kuwapo wahandisi kutoka nje ya Tanzania. Anaamini kuwa kwa kutumia wataalamu wetu waliopo hapahapa Afrika, tunaweza kutumia rasilimali tulizonazo kwa manufaa yetu. Aidha, anapendekeza rasilimali zilizopo Afrika ni vema zikatumika kuendelea viwanda vya Afrika.

Mkakati wa kuwatumia wataalamu wa Kiafrika ili kujiletea maendeleo yao wenyewe umejitokeza pia katika riwaya ya *Mzingile*. Mwandishi anaamini kabisa kwamba, ili kuweza kupata maendeleo ni sharti Waafrika waondokane na dhana potofu ya kwamba maendeleo yataletwa na wageni, bali yataletwa na wao wenyewe. Mwandishi anathibitisha maneno haya katika riwaya yake ya *Mzingile* pale anaposema:

Hakuna taifa ambalo limepata kuendelea kwa kuwadharau wataalamu wake! (uk. 25).

Maelezo hayo yanathibitisha namna Kezilahabi anavyopendekeza ni mkakati upi utumike kukabiliana na dhana potofu kuhusu Afrika na Mwafrika. Kwa maoni yake ni kwamba, ile dhana ya kuwathamini sana wageni na kuwapuza wazawa kunachochea Wafrika kuchelewa kupiga hatua kimaendeleo.

Aidha, katika kukabiliana na dhana potofu kuhusu Afrika na Mwafrika hususani katika namna Mwafrika anavyosawiriwa katika miktadha mbalimbali, Kezilahabi anapendekeza Mwafrika naye asawiriwe katika taswira chanya. Kwa muda mrefu Mwafrika amekuwa akisawiriwa katika taswira hasi katika miktadha mbalimbali. Ili kukabiliana na dhana hii potofu, Kezilahabi katika riwaya yake ya *Nagona* anamsawiri Mwafrika katika mtazamo chanya. Mwandishi anasema:

...Nilipoamka nilinawa uso harakaharaka kama mwanajeshi. Nilipotoka nje watu wengi walikuwa tayari wamekwishaanza maandalizi. Nilikuwa sijui namna ya kujiandaa. Nilikata shauri kumtembelea jirani yangu. **Yeye alikuwa mmojawapo wa watakatifu wa kwanza wa Kiafrika.** Nilimkuta akilemba kofia lake la manyoya (uk. 53) (Maandishi yaliyokolezwa ni msisitizo wa maandishi wa makala).

Maelezo hayo yanadhihirisha mkakati unaopendekezwa na Kezilahabi katika kukabiliana na dhana potofu. Kwa muda mrefu, Afrika na Mwafrika vimekuwa vikisawiriwa katika mtazamo hasi. Kwa mfano, sehemu kubwa ya watakatifu wanaozungumziwa katika vitabu vya dini hakuna watu weusi (Waafrika) wanaojitokeza kuhusishwa na utakatifu. Hii ni dhana potofu ambayo ili kukabiliana nayo mwandishi anaona ipo haja ya kuanza kuisawiri Afrika na Mwafrika katika mtazamo chanya. Kwa mfano, tumekuwa tukisikia majina mengi ya watakatifu ni Wazungu. Sio rahisi kusikia mtakatifu mwenye jina la Kiafrika. Mkakati huu ni kama ule unaopendekezwa na Malugu (2019). Malugu (keshatajwa) katika makala yake anasisitiza kuenzi na kuyasifia mambo yote mazuri yaliyopo Afrika. Anapendekeza kuwa, ikiwezekana hata hoteli maarufu zilizopo Afrika zipewe majina ya Kiafrika badala ya kupewa majina ya kigeni.

Vilevile, katika kukabiliana na dhana potofu kuhusu Afrika na Mwafrika, Kezilahabi anapendekeza Waafrika kutatua matatizo yao wao wenyewe pasipo kusubiri kusaidiwa na wageni. Mwandishi anapendekeza kuwa Waafrika wenyewe ndio wawe chachu ya maarifa ili kukabiliana na mambo yanayowakabili. Haya yanajidhihirisha katika riwaya ya *Mzingile* pale anaposema:

Yasemekana Kakulu alipojiona mzee aliwateua wazee watano, mmoja kutoka kila kijiji akaenda nao msituni. **Huko alikaa nao kwa muda wa mwezi mmoja, akiwafunza historia, mila na desturi, dawa, unajimu na mengine mengi.** Alipoona wamekomaa aliwaongoza hadi chini ya mlima. Kwa mara ya kwanza wakaiona nyumba yake ndogo. Wakiwa juu mlimani aliwaonyesha kwa fimbo yake nchi iliyokuwa chini. “Hii yote ni nchi yenu, msikubali ichukuliwe na watu wageni! Sasa nendeni; waongozeni na wafundisheni watu niliyowafundisha. Mimi nitabaki hapa kuwasha moto utakaomulika dunia nzima (uk. 4) (Maandishi yaliyokolezwa ni msisitizo wa maandishi).

Maelezo hayo yanatupeleka katika mkakati anaopendekeza Euphrase Kezilahabi katika kukabiliana na dhana potofu. Kezilahabi anahimiza kuwa wazee wa Kiafrika hawana budi kuhakikisha mambo yawahusuyo Waafrika yanafundishwa kwa jamii. Mambo muhimu kama vile historia ya jamii, mila na desturi, dawa na unajimu yanarithishwa kutoka kizazi kimoja hadi kingine. Kwa kufundisha kuhusu historia, jamii itafahamu ilikotoka, ilipo na inakokwenda. Mila na desturi itaisaidia jamii kuenzi mfumo mzima wa maisha ya jamii na hivyo kuepuka athari za utamaduni wa kigeni. Aidha, jamii inafundishwa kuhusu dawa mbalimbali zitakazotumika kama tiba badala ya kutegemea dawa kutoka kwa wageni. Unajimu unahusiana na elimu ya anga. Elimu hii ina nafasi muhimu katika jamii za Kiafrika kwani jamii itajifunza kuhusu majira mbalimbali. Maarifa haya yataisaidia jamii kufahamu ni wakati gani wa kulima, kupanda na hata kuvuna.

Mkakati mwingine unaopendekezwa na Euphrase Kezilahabi katika kukabiliana na dhana potofu kuhusu Afrika na Mwafrika ni ule wa kutokubali kujidhalilisha ama kuuza utu wa Mwafrika kwa tamaa ya pesa. Mkakati huu unaenda sanjari na kutukuza vitu kama vile rangi inayosawiri Uafrika kama namna ya kuenzi na kueneza Uafrika. Tukimnukuu mwandishi huyu katika riwaya yake ya *Mzingile* anasema:

Hapa sasa nawaletea Afrika.” Holi zima lilipata kichaa kabla hata hajaingia. **Alivaa vazi jeusi toka blauzi hadi kiatu. Muziki wa kuingilia ulipolia aliingia kwa utaratibu bila kucheza. Alishika kipaza sauti na kwa sauti nyororo akasema, “Mimi ni mwanzo na mwisho wenu. Mlikuwa kupitia kwangu na mtaondoka kupitia kwangu. Kunivunjia mimi heshima ni kujivunjia heshima ya utu wenu. Mimi ni tumaini la mwisho la heshima, utu na uhai wa binadamu.** (kur. 48-49) (Maandishi yaliyokolezwa ni msisitizo wa maandishi wa makala).

Maelezo hayo japo ni machache lakini ndani yake yamefumbata mambo mengi sana. Kwanza kabisa, rangi ya mavazi aliyovaa yanasawiri rangi ya Mwafrika. Mavazi haya yamevaliwa kuanzia vazi la juu hadi viatu. Mavazi haya ni meusi. Rangi nyeusi huashiria Mwafrika. Kezilahabi alikuwa na uwezo wa kumsawiri mhusika huyu akiwa amevaa mavazi ya rangi nyingine yoyote iwayo. Mathalan, mtu mweusi hutakiwa kuvaa nguo nyeupe ama nyingine yoyote lakini sio nguo ya rangi nyeusi. Kitendo cha Kezilahabi kumsawiri mhusika huyu akiwa amevaa vazi jeusi ni dhahiri kabisa kwamba

kuna jambo alilolenga kutuonyesha. Kwa kuwa Kezilahabi amekuwa akitetea utamaduni wa Mwafrika, hapana shaka kwamba alilenga kuupigia chapuo Uafrika. Kwa kufanya hivi Kezilahabi anapingana na dhana iliyopandikizwa inayoufungamanisha weusi na uwi/ubaya ama uovu.

### Akili, Rangi ya Ngozi na Maumbile

Kwa muda mrefu, mtu mweusi (Mwafrika) amekuwa akisawiriwa na mataifa ya Magharibi katika mtazamo hasi. Weusi ya ngozi yake umenasibishwa na taswira hasi. Kwa mfano, hata katika kumsawiri shetani, shetani anaonyeshwa akiwa ni mweusi. Kwa mfano, Afrika liliitwa kuwa ni bara la giza. Giza lililohusishwa na maendeleo, utamaduni, ustaraabu uwezo wa akili na kadhalika. Malugu (2021:60) akimnukuu Robert (1951:10) anasema, “Hekima ni kitu adimu kupatikana kwa mtu asiye na mvi. **Weusi wa nywele za mshitakiwa waonyesha waziwazi ujinga alionao.**” Kulingana na maelezo hayo, nywele nyeusi zinahusianishwa na uwezo mdogo wa akili. Dhana potofu kama hii pia inapatikana katika kitabu cha *The Philosophy of History* cha Hegel (1956) ambapo anadai kuwa, Waafrika ni watu ambao hawakuwa na historia yao wenyewe. Hegel, **aliwachukulia Waafrika sawa na watoto waliodumaa akili** ambao hawangeweza kujiongoza wenyewe bila kuongozwa. Chanzo cha dhana hii potofu kuhusu Afrika na Mwafrika kinahojiwa na King’ei na Amata (2001) katika shairi lao la “Weusi likosa nini?” Katika shairi hilo, waandishi hawa wanauliza kuwa sisi watu weusi tulipataje huo weusi? Na kwa nini weusi upewe sifa mbaya? Kwa nini hata Lusifa apewe sifa ya weusi wakati Adamu na Hawa wamepewa sifa ya weupe? Yesu Mwana wa Mungu na malaika wote ni Wazungu.

Katika kukabiliiana na dhana potofu kuhusu Afrika na Mwafrika, dhana iliyodumu kwa muda mrefu, Kezilahabi katika riwaya zake anamchora Mwafrika katika mtazamo chanya. Kezilahabi hakubaliani na dhana potofu inayomtazama Mwafrika kama kiumbe duni. Anawachora wahusika wake kama watu wenye uwezo mkubwa wa kiakili, na kwake yeye rangi ya ngozi au maumbile sio kigezo cha kupima uwezo wa akili. Anatuhitishia haya katika riwaya ya *Mzingile* anaposema:

Baadaye Kakulu alikuwa mcheza marimba na zeze. Vyombo hivyo viwili alivimudu vizuri. Aliongezea chombo cha nanga katika ujuzi wake mambo yalivyozidi kumwendea vizuri. Alizoea kuzunguka vilabuni akiwapigia walevi. Waliofurahi walimpa pombe ya bure na wengine walimzawadia pesa. Wakati anapiga aliweza kuimba kwa Kiswahili, Kirusi, Kiarabu, Kiingereza, Kifaransa na lugha zingine ambazo hazikueleweka. Mwanzoni, wanakijiji walifikiri ni utani, lakini siku moja alipofika mzungu mmoja kijijini na Kakulu kupata fursa ya kuzungumza naye lugha ya kwao, wanakijiji walimwamini. Upigaji wa muziki ulifuatiwa na uvumi kuwa alikuwa pia mwanasanaa. Alijenga nyumba yake ndogo kilimani ambayo yasemekana ilikuwa nzuri sana. Alichonga vinyago, alisuka mikeka na aliwasuka nywele wanawake. Watu walianza kuiga ufundi wake, hata nyimbo zake ziliigwa. Polepole alianza kupata heshima. Kama si kukosa mke angeweza kuteuliwa kushika nyadhifa mbalimbali (uk. 3).

Nukuu hiyo inatuhitishia namna Kezilahabi alivyomchora Kakulu katika mtazamo chanya. Kakulu anaonyeshwa kama mtu aliyekuwa na uwezo mkubwa wa kumudu kutumia vifaa vya muziki. Uwezo wa kutumia vifaa hivi vitatu sio suala rahisi. Aidha, Kakulu amechorwa kama mtu mwenye uwezo mkubwa sana wa kutumia lugha mbalimbali. Kakulu aliweza kuimba kwa Kiswahili, Kirusi, Kiarabu, Kiingereza, Kifaransa na lugha nyingine. Hali hii inakanusha ile dhana ya kwamba Mwafrika ni mtu mwenye uwezo mdogo wa kiakili. Ujuzi wa kuongea ama kujua lugha mbalimbali sio rahisi kufikiwa na mtu mwenye uwezo mdogo wa kiakili.

### Dini

Mikakati inayopendekezwa na Euphrase Kezilahabi inaweza kudhihirika hasa tukianza kwa kutambua kwamba, mwandishi huyu amekuwa akihoji mambo mengi kuhusu ukamilifu wa dini za kigeni ikiwemo Ukristo hususani Ukatoliki. Mezger (2002:75) anadai kwamba, inaonekana Kezilahabi hashawishiwi na imani ya Romani Katoliki kwamba ina manufaa katika kuelewa maana ya maisha. Kulingana na Kezilahabi, imani za kijadi na imani za kigeni kama Uislamu, Ukristo na Kihindu

kuhusiana na Mungu zinafanana. Kezilahabi anaona kuwa, imani za kigeni ni mwendelezo tu kwa namna iliyoboreshwa wa imani zile za kijadi za tangu kale. Licha ya waamini wa imani za kigeni kujiona ni bora zaidi ya waamini wa imani za kijadi, Kezilahabi anaona kuwa makundi haya mawili yanafanana zaidi kuliko kutofautiana (Mlaga, 2018:13).

Katika kukabiliana na dhana potofu iliyopandikizwa kwa kupitia dini, Kezilahabi anatumia njia ya kuonesha udhaifu wa dini hizi za kigeni kama mkakati wa kukabiliana na dhana hii potofu. Kezilahabi anaonesha kwamba, licha ya kuaminishwa kwamba dini hizi ngeni ni mbadala wa dini mbaya/dhaifu za Kiafrika, bado nazo hazina ukamilifu na wala hazijitoshelizi. Katika kufanikisha azma hii, Kezilahabi anatumia kejeli kama njia mojawapo ya kuonesha udhaifu ama kutokukamilika hata kwa imani hizi za kigeni zilizopandikizwa kwa Waafrika. Anakejeli mfumo mzima wa jinsi watu wanavyosali na kuabudu. Katika riwaya ya *Gamba la Nyoka* Kezilahabi anasema:

Mwezi mmoja ulikuwa umekwishapita. Ilikuwa siku ya Jumapili. Kanisani, watu walikuwa wamejaa. Mama Tinda alikuwa amepiga magoti katika upande wa wanawake. Wengine walikuwa wamekaa. Mama Tinda alikuwa amefumba macho, **bila kucheka** akiomba bado msaada wa Bikira Maria ingawa nyumba yake ilikuwa imeanza kujengwa. **Mama Tinda alikuwa akihesabu zile shanga kwa uangalifu zaidi utafikiri akiruka hata moja atafungwa.** Alikuwa akizihesabu kimoyomoyo. Alipofika vituo alikawia kidogo **kama mpiga ramli ambaye amekaribia kubaini jambo.** Alikuwa sasa amefikia kituo cha tatu. Kituo cha tatu. Yesu alizaliwa katika zizi la ng'ombe. **Tuombe neema ya kupenda umaskini.** Mara alisikia watu wanasimama. Alifumbua macho akaona **'fulani'** amekaribia kusoma Injili (uk. 51) (Maandishi yaliyokolezwa ni msisitizo wa maandishi wa makala).

Katika nukuu hiyo, Kezilahabi anatumia njia ya kejeli katika kuisawiri imani ya dini ya Kikatoliki. Miongoni mwa kejeli zilizotumika ni pamoja na “bila kucheka.” Hapa tunaweza kujiuliza ni kwa nini Kezilahabi aseme Mama Tinda alikuwa amefumba macho akiomba kwa Bikira Maria bila kucheka? Je, kuna sala au maombezi yoyote yanayofanywa na mwombaji huku akicheka? Kwa hivyo basi, tunaona kabisa “bila kucheka” imetumika kwa makusudi kabisa kukejeli imani ya Kikatoliki. Aidha, Kezilahabi kuifaninisha “rozari” na shanga ni mojawapo ya kejeli. Kezilahabi haoni tofauti kati ya rozari na shanga. Katika utamaduni wa Mwafrika hususani maeneo kama ya visiwa vya Ukerewe mahali ambapo Kezilahabi alizaliwa, shanga huvaliwa kiunoni. Kwa Wakatoliki “rozari” inaheshimiwa sana. Sio rahisi kwa mwamini mtiifu wa madhehebu ya Kikatoliki kuifaninisha rozari na shanga. Mbali na maelezo hayo, mwandishi huyu anaona namna waumini wanavyokuwa makini wakati wanasali rozari wanakuwa hawana tofauti na wapiga ramli. Katika jamii za Kiafrika, ramli ilitumika/hutumika katika kubaini tatizo au matatizo yaliyomsibu mtu. Kezilahabi haoni tofauti ya umakini unaowekwa na mtu anayesali rozari na yule anayepiga ramli. Kwa hivyo, kulingana na matumizi ya rozari (shanga kama alivyoziti Kezilahabi) ama kama inavyochukuliwa na jamii ya Kiafrika kama hirizi ni kuwa hakuna tofauti baina ya vitu hivi viwili. Wa Mutiso (2012:115) anaelezea hirizi kuwa:

Hirizi ni kitu kinachomkinga mtu dhidi ya matatizo. Visawe vya neno hili ni ukago (kago), kinga, zindiko, hijabu, pagao, sihiri, uchawi, uganga, (wa kuvaa mwilini), ndumba, mburuga, dunga, urogaji, ulozi, uchomozi, amali, dawa, uwanga, uramali, koma, fingo, n.k. (uk.115).

Hirizi ni kitu chochote kinachoaminika kuwa kinaleta bahati njema au kumkinga mhusika dhidi ya uovu au maovu. Humsaidia anayeimiliki kupata mafanikio, nguvu za kimiujiza, kimaumbile na hata za kiuzazi. Humkinga anayeimiliki dhidi ya hatari zinazodhaniwa kuwepo na mikosi kama kifo, mapepo wabaya, urogi, macho ya husuda, radi kuvunjika kwa chombo cha ubaharia, shambulio la wezi, wanyama hatari, na kadhalika. Warogi, madaktari, manabii, watabiri na waumini huvitumia vifaa hivi katika maisha yao ya kila siku (uk. 116).

Kejeli nyingine inayobainishwa na mwandishi huyu ni pale anaponukuu kituo cha tatu katika rozari “tuombe neema ya kupenda umaskini.” Tunaamini kabisa kwamba, Kezilahabi alinukuu kituo hiki na sio kituo kingine ili kuonesha namna ambavyo dini ya Kikatoliki inavyohalalisha umaskini kama ni kitu kizuri. Hata hivyo, katika *Chuo Kidogo cha Sala: Sala na Nyimbo* (1982) haielezwi



kama ni kuupenda “umaskini” bali “kujaliwa moyo wa ufukara.” Kezilahabi amekibadilisha kifungu hiki kwa makusudi ili kuonesha namna ambavyo dini ya Kikatoliki inavyohalalisha umaskini kama ni jambo zuri. Kukubali umaskini maana yake ni kukubali hata kutawaliwa kwa kuona kwamba sio jambo baya kuwa maskini kwani inakubalika hata kwa Mungu mwenyewe. Mbinu hii ilitumiwa na wageni kama vile wakoloni pindi walipokuja kumtawala Mwafrika. Dini ilitumika kama nyenzo ya kuhalalisha kutawaliwa, kuporwa na kukandamizwa Mwafrika kwa kumjengea hali ya kuwa mnyenyekevu. Ni katika mazingira haya, Kezilahabi anaonesha udhaifu wa viongozi wa madhehebu ya Kikatoliki. Kezilahabi anapoweka msisitizo katika neno, ‘fulani’ katika sentensi, “Alifumbua macho akaona ‘fulani’ amekaribia kusoma Injili,” huyu fulani alikuwa akimrejelea Padri Madevu, Padri aliyekuwa na uhusiano wa kimapenzi na Mama Tinda licha ya kuwa misingi ya kanisa lake haikuruhusu padri kuoa ama kuzini. Pia, yeye kama mtumishi wa Mungu hakupaswa kujiingiza kwenye uzinzi, kwani mapadri wanapaswa kuwa mfano wa kuigwa kwa waumini wao ili kutekeleza yale wanayowahubiria waumini hao.

Mkakati mwingine anaoupendekezwa Euphrase Kezilahabi katika kukabiliana na dhana potofu kuhusu Afrika na Mwafrika kupitia dini anauelekeza katika kuvipuuza hivyo vinavyoitwa vitabu vitakatifu ama vitukufu. Kulingana na Kezilahabi, haoni sababu tena ya kuendelea kuvitumia vitabu hivi yaani *Biblia Takatifu* na *Kurani Tukufu*. Hii ni kwa sababu anaviona ni vitabu vinavyotufumba midomo tuiseme hata pale tunapoonewa. Katika riwaya ya *Nagona*, mwandishi anasema:

Katika mkono mmoja alikuwa amepakatishwa Biblia Takatifu na mwingine Koran Tukufu. Mdomo wake ulikuwa umefungwa kwa kitamba cheupe na juu ya kitambaa hiki kwenye mdomo palionekana maandishi yaliyosema “Kimya ni hekima.” (uk. 3).

“Nilion maiti ndani ya nyumba fulani.” “Alikuwa mjinga.” Alikataa kutupa vitabu vyake. “Walimuua.” “Nani?” “Wanamji.” (uk. 5).

Maelezo hayo tuliyo yadondoa yanatuonyesha udhaifu uliomo katika vitabu vya dini tulizopandikiziwa. Mwandishi anawahimiziwa Waafrika kuachana na vitabu hivyo walivyoaminishwa kuwa vina ukweli mkamilifu. Kwa mfano, dini zinawazuia watu kusema licha ya kuwa, mwanadamu ameumbwa akiwa huru, na anapaswa kuwa huru kusema au kuuliza.

Vilevile, mkakati mwingine unaopendekezwa na Euphrase Kezilahabi katika kukabiliana na dhana potofu kuhusu Afrika na Mwafrika unapitia katika taratibu za kuungama kwa padri. Kutokana na kupuuzwa kwa dini za Kiafrika na kupandikiziwa dini ngeni miongoni mwazo ikiwa ni Ukristo, Kezilahabi anaonesha mapungufu katika imani ya dini hizi ngeni. Huu ni mmojawapo wa mkakati unaolenga kuwarejesha Waafrika katika imani zao za asili. Kezilahabi anakejeli imani waliyojengewa waumini wa madhehebu ya Kikatoliki ya kuungama dhambi zao kwa padri. Kezilahabi anamsawiri padri kama mwanadamu mwenye mapungufu ya kibinadamu sana sawa na binadamu wengine na kwa hivyo hana utakatifu wowote kama waumini wanavyoaminishwa. Kwa mfano, anataeleza kwamba, dhambi za mhusika hazikuweza kusamehewa kwa kuwa aliungama dhambi zake kwa padri ambaye ni mlevi. Tukimnukuu mwandishi katika riwaya ya *Nagona* anasema:

“Lakini niliungama dhambi zangu zote. Dhambi za karne na karne. Nilikiri makosa yangu!”  
“Najua. Lakini ulipoteza muda wako. **Hukusamehewa hata dhambi moja.**” **“Uliungama kwa padri mlevi. Watu kama hao huwa hawasikilizwi. Baraka zao huishia katika kufukuza tu nzi nyusoni pao.”** Lakini mimi binafsi nilikiri makosa yangu. Hiyo inatosha, padri si kiunganishi tu?” **“Uzushi!** Hoja ilikuwa kubadili vitendo vyako na fikra zako kulingana na umri wa mtoto wetu!” (kur. 16-17) (Maandishi yaliyokolezwa ni msisitizo wa maandishi wa makala).

Dondoo hilo linaeleza kitendo cha kuungama kwa padri kama uzushi aliopandikiziwa Mwafrika ambao unapaswa kuepukwa. Mwandishi anaita ni uzushi kwa kuwa padri huyu anayeaminika kuwaondolea watu dhambi, yeye mwenye ni mlevi. Yaani ana mapungufu sawa au pengine zaidi ya yule anayemuomba. Kwa maelezo hayo, Kezilahabi haoni sababu ya watu kuendelea kuungama dhambi zao kwa mapadri.

Kwa namna nyingine, katika kukabiliana na motifu za dhana potofu kuhusu Afrika na Mwafrika, Kezilahabi anaonesha udhaifu wa waanzilishi wa imani, itikadi na mifumo mbalimbali ambayo Waafrika walipandikiziwa ili kuifuata na kuiamini. Hawa ni waasisi wa dini za Kikristo na Kiislamu. Lakini pia wapo wanafalsafa na wachumi ambao walianzisha mawazo mbalimbali ambayo yaliulazimu ulimwengu mzima kufuata mawazo yao. Katika riwaya ya *Nagona*, Kezilahabi anaeleza kama ifuatavyo:

Mashujaa wote wamezikwa katika kilima hiki, hapa! Lile pale mlionalo kama pango, yasemekana ni kaburi la Yesu. Lile pale lenye udongo mwingi ni la Muhammad. Hapo mlipokanyaga ni kaburi la Marx, na lile pale ni la Socrates. Mnajua tena ng'ombe wa hapa hawana cha mswalie mtume. Hawaishi kuyakwaruza makaburi haya kwa kwato na kuyagongagonga kwa pembe. Kaburi la Marx limekwanguliwa na limeanza kufifia. Na mbwa hawana adabu. Hapana siku ipitayo bila ya kuyakojolea makaburi haya. Yasemekana wanaweka alama zao wasipotee njia wakati wa kurudi safarini." Kimya kilifuata. Tulikuwa tumechanganyikiwa. Kila tulichokiona kilionekana kuwa cha ajabu. Kizee kiliendelea: "ajabu ni kwamba wezi, majambazi, maskini, vipofu, walawiti na vichaa ndio wafikao mara moja kwa mwaka kuyapalilia. (uk. 19).

Dondoo hili limefumbata mambo mengi sana yanayoelezwa na Kezilahabi, ambayo yanaweza kuchukuliwa kama sehemu ya mkakati wa kukabiliana na dhana potofu kuhusu Afrika na Mwafrika. Inafahamika kwamba, kaburi la Yesu lilikuwa kwenye pango. Pia, kaburi la Muhammad kama tunavyofahamu katika makaburi ya Waislamu, makaburi yao hurundikiwa udongo mwingi kwa juu. Mbali ya makaburi ya Yesu na Muhammad kuonyeshwa jinsi yalivyokuwa, pia tunaonyeshwa kaburi la Marx. Lakini kaburi hili la Marx, ni kaburi ambalo tumelikanyaga sasa. Kulikanyaga kaburi la Marx sasa, yaani kuwa ndipo tulipo kwa wakati huu, inarejelea nyakati ambazo kitabu hiki kilikuwa kimeandikwa. Kilikuwa ni kipindi ambacho bado mawazo ya Marx yalikuwa yameshika hatamu, licha ya mwanzilishi wa mawazo hayo kuwa aliishafariki. Kaburi la Socrates linaonekana kuwa mbali kidogo na mahali tulipo. Hii inarejelea kuwa, Socrates aliishi miaka ya awali kabla ya Marx, ndiyo maana tunaambiwa "lile pale" kuashiria mbali kidogo, tofauti na "hapo mlipokanyaga." Kaburi la Socrates kuoneshwa kuwa lipo mbali kuliko kaburi la Marx kunaashiria mawazo ya Socrates ni ya kitambo yakilinganishwa na ya Marx. Mwanzoni kabisa, Kezilahabi anaeleza kuwa, mashujaa wote hao tayari wameishazikwa. Hii pengine huweza kuashiria kwamba, wao kama walivyozikwa, mawazo yao pia yamezikwa ama yanapaswa kuzikwa/kusahaulika. Kukwanguliwa kwa kaburi la Marx na kuanza kufifia, kunarejelea mawazo ya Marx ambayo licha ya kwamba ndiyo mawazo yaliyoibuka mwishoni kuliko ya Socrates, nayo sasa yameanza kufifia ama kupuuzwa.

Aidha, Kezilahabi anatwambiwa kwamba, makaburi hayo, yaani la Yesu, Muhammad, Socrates na Marx, wezi, majambazi, maskini, vipofu, walawiti na vichaa ndiyo wafikao mara moja kwa mwaka kuyapalilia. Pengine, hapa tunaweza kusema kuwa, kwa kurejelea nafasi waliyo nayo katika jamii watu hawa ambao hasa ndio huenda kuyapalilia makaburi hayo, tunaona ni nafasi duni kabisa. Ni makundi ya watu wenye hadhi ya chini, tena wanaodharaulika kabisa. Hapa ni kana kwamba Kezilahabi anatwambia, mawazo ya waasisi hao tuliyoyataja ni kama yamepitwa na wakati na ndio maana hata wafuasi wake (watu wanaoenda kuyapalilia makaburi hayo ni watu wa hadhi ya chini katika jamii) huu ni mkakati mwingine unaowaamsha Waafrika kuepukana na kufungwa na mawazo pamoja na mitazamo ya watu ambao tayari hawapo tena duniani. Kufa kwao maana yake na mawazo yao yamekufa. Na hapa ndipo Kezilahabi anapotusisitiza kwamba katu

Vilevile, kama sehemu ya mkakati wa kukabiliana na dhana potofu zilizopandikizwa kuhusu dini za Kiafrika, Kezilahabi anaonesha kupwaya kwa imani za dini za Kikristo na Kiislamu kama suluhisho la kutatua matatizo ya watu. Kupwaya huku kunapendekeza Waafrika kurudi tu katika imani zao za asili, kwani imani hizi ngeni bado zimeshindwa kutatua changamoto au matatizo yanayowakumba watu. Katika riwaya ya *Mzingile*, mwandishi anasema:

Halafu kuna kisa cha huyu padiri mzungu. Alisali akasali wee! Wapi! Ukame haukwisha. Katika hali ya kukata tamaa, alipoona waumini wanaanza tena kutoa makafara mbuyuni,

alianza kunywa sana pombe kali za kwao. Zilipokwisha akanywa gongo. Katika ulevi wake alivunjavunja baadhi ya masanamu kanisani. Alisikika akipiga kelele. “Mungu gani wewe! Umeniaibisha mbele ya watu weusi!” alipoanza kuchanganya gongo na mvinyo, masista walimkimbia. Gongo tupu lilikuwa halimpi nishai ya kutosha. Alianza sasa kuhubiri juu ya dini mpya, ambayo ni tokeo la muungano kati ya Biblia na Kurani, vitabu alivyokuwa akisoma sana wakati huo (uk. 24)

Shekhe ndiye aliyewachekesha watu. Alipoona mambo yanazidi kuwa mabaya alijiotea visichana vidogo vitano, akidai pepo huanzia hapahapa ulimwenguni. Waliwaita mahurulaini. Waumini wake wakafuatia. Lakini kutokana na hali halisi Uislamu ulibaki jina. Wanyama wengi walijifia tu. Wao pia wakala nyamafu. Walifikia hatua ya kuchezea bao msikitini ili kujisahaulisha njaa. Binadamu walipoanza kulana wenyewe kwa wenyewe, msikiti uliota nyasi hata paani. Nguvu za kujitafutia zilipomwisha mahurulaini walimkimbia Sheikh. Siku moja fisi mwenye njaa aliingia nyumbani mwake. Shekhe hakuwa na nguvu za kujinyanyua mwenyewe. Fisi alimtishia akaona hatingishiki wala kustuka. Sheikh alianza kumwomba fisi, “tafadhali kwa jina la Allah usinile.” Fisi alimtishia mara ya pili. “Tafadhali kama lazima unile basi nile kuanzia miguuni.” Fisi alitishia mara ya tatu. Alipoona kimya aliingiza meno yake tumboni. Nusu dakika utumbo wote ulikuwa umekwisha. Alimburura nje. Fisi wengine wakajongea. Majirani walisikia tu mifupa ikilia katika meno ya fisi huku wakicheka (kur. 24-25).

Katika madondoo haya mawili, Kezilahabi anaonesha namna ambavyo dini za Kikristo na Kiislamu zinavyoshindwa kuwa mbadala wa matatizo ya watu, na hivyo kuhitajika mbadala mwingine ambao utakuwa ni kuibuliwa kwa dini mpya ambayo siyo Ukristo wala Uislamu. Mwandishi anatuonesha namna ambavyo Ukristo kwa kupitia kwa padiri unavyoshindwa kutatua tatizo la ukame hali iliyosababisha waumini warudi katika dini ama imani zao za asili kama mbadala wa kukabiliana na ukame. Hali hii ilimfanya padiri mwenyewe kuonesha kwamba kumbe huyo Mungu ambaye imani yake imepandikizwa kwa Waafrika bado hana msaada kwa Waafrika. Na hapa ndipo alipoanza kuhubiri dini mpya, dini ambayo ni tokeo la muungano wa Biblia na Kurani. Dini hii mpya ndiyo iliyokuwa ikisisitizwa na Kezilahabi kama mbadala wa dini za Kikristo na kiislamu ambazo kulingana na mtazamo wake hazina nafasi tena kwa maisha ya Waafrika.

Kezilahabi haishii katika Ukristo tu katika kupendekeza mkakati wa kukabiliana na dhana potofu zilizopandikizwa kwa Mwafrika. Kezilahabi anatazama pia kushindwa kwa dini ya Kiislamu katika kutatua matatizo ya watu kupitia kwa Shekhe. Shekhe naye mambo yalipomzidia aliamua kuachana na misingi ya dini yake na kujipa matumaini kwamba hata duniani pawweza kuwa peponi. Mawazo kama haya pepo kuweza kuwa hata hapa ulimwenguni ni kama yale tuliyoyaona katika sehemu iliyotangulia katika shairi la Mulokozi la “Mimi ni Nani” linalopatikana katika kitabu cha *Kunga za Ushairi na Diwani Yetu* (1979). Katika shairi hili, Mulokozi anaamini maisha mema na mabaya yatategemea na jinsi unavyoishi duniani. Kwa maneno mengine, duniani panaweza kuwa ndiyo pepo yako ikiwa unaishi maisha ya raha. Lakini pia jehanam yako inaweza kuwa ni hapahapa duniani kama unaishi maisha magumu.

Kwa hivyo, Shekhe na waumini wake walilazimika kuuacha Uislamu na kukiuka misingi ya imani ya Kiislamu kama ile inayowazuia kula nyamafu nao wakaanza kula nyamafu. Walianza hadi kucheza bao msikitini. Msikiti ulisahaulika hadi nyasi zikaota. Cha kushangaza hata pale alipotaka kuliwa na fisi na akiita jina la Allah (Mungu) bado aliliwa na fisi. Hali hii inaendelea kutudhihirishia namna ambavyo dini za kigeni zilizopandikizwa kwa waafrika zinavyoshindwa kutatua matatizo ya watu. Hapa ndipo Kezilahabi anaposisitiza kuachana na dini hizi walizopandikiziwa Waafrika kwani hazina msaada tena kwao. Kwa hivyo, Waafrika wanapaswa waibue dini nyingine ambayo itakuwa suluhisho la matatizo yao badala ya Ukristo na Uislamu.

Katika kukabiliana na dhana potofu kuhusu Afrika na Mwafrika, Kezilahabi anajaribu kulinganisha nguo na zana zilizotumika katika ibada za Kikristo kuwa ni sawa na zile za matambiko. Haya yanajitokeza katika riwaya ya *Mzingile* pale anaposema:

Nilifungua madawati yaliyokuwa humo. **Yote yalikuwa yameenea nguo na zana zingine za matambiko.** Katika kabati moja, nilikuta chupa nyingi za mvinyo. Nilichukua chupa mbili nikatoka nje (uk. 65). (Maandishi yaliyokolezwa ni msisitizo wa maandishi wa makala).

Kutokana na dondoo hilo, Kezilahabi haoni tofauti kati ya zana na nguo zilizotumika katika ibada za Kikristo kuwa sawa na zile za matambiko yaliyofanywa na Waafrika. Katika matambiko na ibada za Kiafrika, kulikuwapo na mavazi maalumu yaliyoteuliwa kwa ajili ya shughuli husika. Vivyo hivyo, katika ibada za Kikristo, mavazi na zana ziliteuliwa kutegemeana na shughuli husika ya kiibada iliyokuwapo siku hiyo. Kwa mfano, nguo ambazo zingevaliwa na kiongozi wa ibada katika shughuli za mazishi, katu hazingeweza kufanana na zile ambazo zingevaliwa siku ya maadhimisho ya siku ya Pasaka. Matambiko anayorejelea hapa Kezilahabi ni sawa na yale yanayopatikana katika jamii za Kiafrika. Matambiko haya yalikuwa ni sehemu ya ibada za kijadi za kijamii. Ni matambiko hayahaya anayozungumzia Kezilahabi ambayo baada ya kuingia kwa wageni waliyapuuza na kuyaita ni sehemu ya ibada na utamaduni wa kishenzi. Ni utaratibu uliotazamwa kama utamaduni au imani mbaya ambao ulipaswa kupigwa vita kwa hali na mali.

Kadhali, katika kukabiliana na dhana potofu, Kezilahabi anapingana na wazo alilopandikiwa Mwafrika kutokana na imani za kigeni. Imani hizi ni zile zinazomwaminisha kwamba, peponi ni mahali fulani maalumu. Tena, anaona kabisa kwamba, chanzo cha matatizo anayoyapata mwanadamu yanatokana na kitendo cha Mungu kuwafukuza wanadamu katika bustani waliyokuwa wakiishi. Tukimnukuu Kezilahabi katika riwaya ya *Mzingile* anasema:

“Lakini maisha yaliyokwisha yalianza hivi hadi kufikia vurumai!” “Hayo yalianzia katika ndoto za mzee, yakawa mabaya zaidi alipoamka na kuwafukuza kutoka bustanini. Haya yanaanzia katika ndoto ya utupu kwenye chemichemi na kuimarishwa na kutoweka kwake. Uzee wake uliruhusu kubomoka na kukataliwa kwa misingi iliyopita, na sasa tunayo nafasi ya kuweka misingi mipya. Hii ndiyo sayansi. Sayansi haifuati ujenzi wa tofali juu ya jingine.” Kimya. “Hapa tuko wapi hasa?” Aliniuliza, “Paradiso?” “Mahali popote panaweza kuwa paradiso ukipatunza vizuri na ukiishi kwa amani ya kudumu.” “Hiyo amani inapatikana wapi?” “Ndani mwetu. Mimi na wewe.” (kur. 79-80).

Kama mkakati wa kukabiliana na dhana potofu, Kezilahabi anakosoa kitendo cha Mungu kumfukuza mwanadamu katika bustani ya Edeni. Anaona kwamba, maisha ya mwanadamu yalianza kuwa magumu pindi tu mwanadamu alipofukuzwa katika bustani hiyo. Anatudhihirishia lawama pale anaposema, “Yakawa mabaya zaidi pale alipoamka na kuwafukuza kutoka bustanini.” Matumizi ya neno “alipoamka na kuwafukuza” yawezekana kulingana na Kezilahabi ni kama anashusha shutuma kwa Mungu, kwamba kilikuwa ni kitendo cha kukurupuka tu pasipo kutafakari matokeo ya baadaye ya mwanadamu. Pia, yanaweza kurejelea kitendo cha kukosa huruma ambako hasa ndiko kunakomsababishia mwanadamu zahama katika nyakati hizi za sasa. Matatizo yote haya yanayomkumba mwanadamu, Kezilahabi anayaelekeza kwa Mungu. Anasema yanaanzia “katika ndoto ya utupu.” Ndoto hii ya utupu anayorejelea ni ile ya baada ya mwanadamu kula tunda alilokatazwa na hatimaye akajigundua yupo uchi. Hapo ndipo Mungu alipomlaani mwanadamu na kumfukuza katika bustani ya Edeni, mahali ambapo mwanadamu alikuwa akiyafurahia maisha. “Uzee wake uliruhusu kubomoka na kukataliwa kwa misingi iliyopita, na sasa tunayo nafasi ya kuweka misingi mipya.” Kauli hii inaweza kurejelea maamuzi aliyoyafanya Mungu ya kumfukuza mwanadamu katika bustani ya Edeni ni kama kitendo cha kutokufikiria; yaani uzee. Uzee huu (kutokuchukua maamuzi sahihi) kumempa mwanadamu wasaa sasa wa kumchambua Mungu na kumtafakari, na mwisho kuona kama hana nafasi kubwa tena kwa maisha ya mwanadamu. Hali hii ilisababisha kuchochewa kwa kuwekwa misingi mipya. Misingi hii ndiyo ile inayowekwa na wadhanaishi kama akina Martin Heiddiger, Friedrich Nietzsche na wengineo ambao hawaoni tena nafasi ya Mungu katika maisha ya mwanadamu. Wanaamini kabisa, maisha ya mwanadamu yanaweza kuwa bora iwapo mwanadamu ataacha kumtegemea Mungu. Wanahimiza kufuata njia za kisayansi katika kukabiliana na changamoto au matatizo mbalimbali yanayomkabili mwanadamu badala ya kumtegemea Mungu. Na kwa kuwa tayari mwanadamu aliishafukuzwa Paradiso, asitarajie

tena kuiona Paradiso hiyo. Kwa hivyo, kulingana na Kezilahabi, mwanadamu ana jukumu la kujiandalia Paradiso yake mwenyewe. Tena, Paradiso hii siyo lazima iwe ni mbinguni. Hata hapa duniani panaweza kuwa Paradiso iwapo mwanadamu ataboresha namna yake ya kuishi na kudumisha amani. Mawazo kama haya yanafanana na mawazo ya Mulokozi (1979:76) katika kitabu cha ushairi cha *Kunga za Ushairi na Diwani Yetu* shairi la “Mimi ni Nani,” ambapo haamini kama kuna Mungu wala mbingu. Zaidi, anaamini roho yako ndiyo Mungu wako, na mateso yako duniani ndiyo Jahanam yako. Hii ina maana kwamba, iwapo mtu ataweza kuishi maisha mazuri duniani, tena yenye amani, basi hiyo ndiyo pepo. Kwa hivyo, Kezilahabi haoni sababu ya mwanadamu kupotoshwa kwamba mbinguni pekee ndiyo Paradiso kama mahubiri na mafundisho ya Ukristo na Uislamu yanavyoelekeza. Kwa maelezo haya, tunaweza kusema kwamba, Kezilahabi anajaribu kuwashawishi Waafrika kuachana na imani waliyopandikiziwa na wageni. Imani ambayo nayo kimsingi haitoi suluhu ya kweli kwa changamoto na maisha magumu anayoyapitia mwanadamu. Anahimiza kwamba, ni jukumu la mwanadamu mwenyewe kujiandalia maisha yake mema ikiwemo Paradiso.

Aidha, katika maelezo tunayoyapata katika dondoo letu hapo juu kutoka riwaya ya *Mzingile* ni kwamba, kitabu cha *Das Kapital* ambacho hapo awali kilikuwemo kanisani wakati wa kubomoa magofu hakikuonekana tena. Kitabu hiki kiliandikwa na Karl Marx. Inafahamika kwamba, Marx ni miongoni mwa watu walioibuka na kupingana na dini. Kimsingi, mawazo ya Marx yalikuwa ni kama kaa la moto kwa waamini wa Ukristo na Uislamu. Mawazo ya Marx yalichambua imani na mafundisho yaliyokuwa ndani ya dini hizi na kuyatoa dosari nyingi. Kwa hivyo, mawazo ya Marx hayakukubalika katika imani ya dini hizi mbili alizopandikiziwa Mwafrika. Pengine, ilionekana mawazo ya Marx yangewachochea waamini wa dini hizi mbili kupunguza ufuasi wao au kuachana kabisa na dini hizi. Njia pekee ya kukabiliana na mawazo ya Marx ilikuwa ni kutengeneza mazingira ya kuyafutilia mbali mawazo hayo kwa waumini wa madhehebu hayo. Yawezekana ndiyo maana kitabu cha *Das Kapital* ambacho kilikuwa kanisani, wakati wa kubomoa magofu na kuvichoma vitabu vya misingi ya imani ya Kikristo na Kiislamu, tayari kitabu hicho kilikuwa kimeishateketezwa kabla.

Namna nyingine inayopendekezwa ya kukabiliana na dhana potofu zilizopandikizwa kwa Mwafrika inayowazungumzia watakatifu wote kuwa ni watu weupe, ni kuwasawiri Waafrika nao kwa namna hiyo. Katika kupandikiza dhana potofu, wageni walihakikisha kwamba, hakuna namna ambayo Waafrika walisawiriwa kama watakatifu. Ili Mwafrika aonekane ni mtakatifu alipaswa achukue jina la Kizungu. Tukimnukuu mwandishi katika riwaya ya *Nagona* anasema:

Nilikata shauri kumtembelea jirani yangu. Yeye alikuwa mmojawapo kati ya watakatifu wa kwanza wa Kiafrika. Nilimkuta akilemba kofia lake la manyoya (uk. 53).

“Wewe ni kiongozi?” “Ndiyo. Kila mtakatifu atawaongoza wale wote waliochagua jina lake ngomani.” “Viongozi wengi watakuwa wazungu kwani watu wengi ulimwenguni wamechukua majina yao.” Ni kweli. Hii ni kwa kuwa wamekuwa mabingwa wa kucheza ngoma kwa muda wa karne nyingi. Sisi tulikuwa tukifuata nyayo zao.” ... “Wapagani je, watakuwa wapi?” “Kwa nini! Wao pia wana majina. Kama jina lako ni Chokoa basi utafuatana na Chokoa wa kwanza. Vivyo hivyo, kwa majina ya dini nyingine, Khamis, Cheng Hao na kadhalika. Lakini inasemekana kwamba wapagani watapangwa mbali sana na kitovu cha duara.” (uk. 54).

Katika dondoo hili, Kezilahabi anajaribu kukabiliana na dhana potofu kwa kuonesha kwamba, kumbe hata Mwafrika anaweza kuwa mtakatifu. Kuwa mtakatifu siyo lazima tu uwe Mzungu au uchukue jina la Kizungu. Kezilahabi anapingana na dhana ya kuwaita Waafrika ambao hawajakubaliana kufuata imani za kikristo na Kiislamu kuwa ni wapagani. Hawa wanoitwa wapagani, kimsingi, wana majina yao. Anaonesha kuwapo kwa uvumi unaoenezwa kwamba, siku ya mwisho Waafrika ambao watakuwa hawajakubali kufuata imani ya kigeni watatengwa mbali sana. Anapingana kwa kudai kwamba, kama kigezo cha kuwa karibu na duara ni kutokana na kuwa na jina, hata hao wanaoitwa kuwa ni wapagani wana majina yao.

### Hitimisho

Euphrase Kezilahabi kwa kupitia riwaya tatu tulizozirejelea amedhihirisha namna anavyojaribu kukabiliana na dhana potofu zilizopandikizwa na wageni kuhusu Afrika na Mwafrika. Ametumia mbinu ya kejeli kuonesha namna lugha za kigeni zinavyoshindwa kutimiza malengo ya elimu kwa Waafrika. Pia, ameonesha namna Mwafrika anavyoweza kuwa na vipaji vingi kwa kumtumia mhusika Kakulu. Vilevile, Kezilahabi amesisitiza Waafrika wao wenyewe wanapaswa wajishughulikie mambo yanayowahusu badala ya kusubiri kutimiziwa na wageni kutoka Afrika. Kezilahabi katukumbusha uzuri wa kuuthamini weusi wetu kuanzia kwenye mavazi hadi rangi ya ngozi. Ametukumbusha pia kuwa Afrika ndiyo chimbuko la Mwanadamu na kwa hivyo Afrika na Mwafrika hawapaswi kupuuzwa. Mkakati mwingine alioupendekeza na kuusawiri kwa marefu na mapana ni ule unaohusiana na dini. Katika kutaka kuwarejesha Waafrika kutafakari upya dini ne imani ngeni walizopandikiziwa na wageni, ameonesha kufanana kwa baadhi ya mambo ya dini za kigeni na yale ya jadi. Pia, ameonesha udhaifu wa dini za kigeni huu ukiwa ni mkakati wa kuwataka Waafrika walizitathmini upya dini hizi pamoja na mafundisho yake. Kwa jumla, Kezilahabi ametumia mbinu ya kuonesha mapungufu katika dhana alizopandikiziwa Mwafrika lengo hasa likiwa ni kuzitathmini na kuchukua hatua.

### Marejeleo

- Berg, L. B. (2001). *Qualitative Research Methods for the Social Sciences* (4<sup>th</sup> ed.). Boston and London: Allyn and Bacon.
- Bible Society of Tanzania. (1997). Biblia Maandiko Matakatiifu, *Mwanzo*. Dodoma: Bible Society of Tanzania.
- Bible Society of Tanzania. (1982) *Chuo Kidogo cha Sala: Sala na Nyimbo*. Peramiho: Peramiho Publications.
- Hegel, G. F. (1956). *The Philosophy of History*. New York: Dover Publications.
- Iribemwangi, P. I. na Mukhwana, A. (2011). *Isimujamii*. Nairobi: Focus Publishers Ltd.
- Kezilahabi, E. (1974). *Kichomi*. Nairobi: Heinemann Educational Books (E. A) Ltd.
- Kezilahabi, E. (1990). *Nagona*. Dar es Salaam: Dar es Salaam University Press.
- Kezilahabi, E. (1991). *Mzingile*. Dar es Salaam: Dar es Salaam University Press.
- Kezilahabi, E. (2006). *Gamba la Nyoka*. Nairobi: Vide~Muwa Publishers Limited.
- King'ei, K. (2010). *Misingi ya Isimujamii*. Dar es Salaam: Taasisi ya Taaluma za Kiswahili, Chuo Kikuu cha Dar es Salaam.
- King'ei, K. na Amata, J. K. (2001). *Taaluma ya Ushairi*. Nairobi: Acacia Stantex Publishers.
- Malugu, A. (2019). 'Motifu za Dhana Potofu kuhusu Afrika na Mwafrika: Mifano kutoka Riwaya ya *Njama* (A. E. Musiba) na *Tutarudi na Robo Zetu?* (Ben R. Mtobwa)? *Lugha na Fasibi katika Mshikamano wa Kitaija na Uviano Barani Afrika*. Eldoret: Moi University Press.
- Malugu, A. (2021). 'Istara katika Riwaya ya *Kusadikika* ya Shaabani Robert.' *Mwanga wa Lugha*, Juzuu 5 Aprili. Moi: Moi University Press.
- Meinhof, C. (1915). *An Introduction to the Study of African Languages*. London and Toronto: J. M. Dent and Sons Ltd.
- Mezger, S. (2002). 'Roman Catholic Faith Represented in Kezilahabi's Mzingile' in *Swahili Forum X*. 75-85.
- Mlaga, W. K. (2018). 'Euphrase Kezilahabi kama Mwanafalsafa Kamili: Mifano kutoka Riwaya ya Mzingile' katika *Mulika* Na. 37. Dar es Salaam: TATAKI.
- Mulokozi, M. M. na Kahigi, K. K. (1979). *Kunga za Ushairi na Divani Yetu*. Dar es Salaam: Tanzania Publishing House.
- Njogu, K. na Chimerah, R. (1999). *Ufundishaji wa Fasibi; Nadharia na Mbinu*. Nairobi: Jomo Kenyatta Foundation.
- Omari, C. K. (1981). *Urithi wa Utamaduni Wetu*. Dar es Salaam: Tanzania Publishing House.
- Robert, S. (1951). *Kusadikika*. Nairobi: Nelson.
- Senkoro, F. E. M. K. (1995). 'E. Kezilahabi: Shaaban Robert wa Pili' katika *Kioo cha Lugha, Juzuu 1*. Dar es Salaam: TUKI. Kur 61-69.
- Wafula, R. M. na Njogu, K. (2007). *Nadharia za Ubakiki wa Fasibi*. Nairobi: Jomo Kenyatta Foundation.
- Wamitila, K. W. (1995). 'Nagona and Mzingile: Kezilahabi's Metaphysics' katika *Kiswahili* Vol. 58. Dar es Salaam: TUKI. Kur 62-67.

Wamitila, K. W. (1997). 'Contemptus Mundi and Carpe Diem Motifs in Kezilahabi's Works' katika *Kiswahili*, Juzuu 60. Dar es Salaam: TUKI. Kur 15-24.

Wamitila, K. W. (2002). *Uhakiki wa Fasih: Misingi na Vipengele Vyake*. Nairobi: Phonex Publishers Ltd.

Wamitila, K. W. (2003). 'Influence or Intertextuality? A Comparative Study of Kezilahabi's Nagona and Mzingile and Juan Rulfo's Pedro Paramo' katika *Kiswahili*, Juzuu 66. Dar es Salaam: TUKI. Kur 49-55.

Wa Mutiso, K. (2012). Motifu ya Hirizi katika Ushairi wa Kiislamu wa Kiswahili katika *Mulika*, Juzuu 31. Dar es Salaam: TATAKI. Kur 115-135.

